# PROGRAMU YA KUJENGA UWEZO WA UFUATILIAJI NA TATHMINI



# MAFUNZO YA UFUATILIAJI UTEKELEZAJI WA MPANGO MKAKATI

TSSL
TWV STRATEGIC SOLUTIONS LIMITED

## UTANGULIZI

Katika kipindi cha miaka kumi, Tanzania imepiga hatua kubwa katika utambuzi, uratibu, na uingizwaji wa mifumo ya ufuatiliaji na tathmini kwenye taasisi na mashirika ya umma. Kasi hii inachochewa na azma ya Serikali ya kuanzisha na kudumisha mifumo madhubuti ya kupima utendaji kazi katika utekelezaji wa sera, mipango, mikakati na miradi.

Moja ya changamoto kuu zinazokwaza uratibu na uingizwaji mzuri wa mifumo hiyo ni upungufu wa uwezo wa kitaalamu katika baadhi ya taasisi za serikali na mashirika ya umma, hali inayochangiwa na ukosefu wa programu mbalimbali, mahususi, endelevu, na za kivitendo za kujenga uwezo ya ufuatiliaji na tathmini .

Ni kwa sababu hiyo TWV Strategic Solutions Limited (TSSL) imeandaa programu maalum ya kujenga uwezo wa ufuatiliaji na tathmni ya utekelezaji wa sera, mipango, mikakati na miradi. Programu hii inalenga kuunga mkono jitihada za wadau mbalimbali katika eneo hili kwa kutoa mafunzo ya ana kwa ana ya wiki moja, yakifuatiwa na kipindi cha uelekezi na ushauri wa karibu kwa washiriki kupitia majukwaa ya mtandaoni na mawasiliano ya simu. Programu hii ina sehemu kuu tatu. Sehemu ya kwanza inahusu kujenga uwezo wa ufuatiliaji wa mpango mkakati wakati ya pili inajikita kwenye miradi ya maendeleo. Tathmni ya miradi ya maendeleo inaaungukia kwenye sehemu ya tatu ya programu hii. Kipeperushi hiki kinahusu sehemu ya kwanza ya programu.

## MALENGO YA MAFUNZO UFUATILIAJI

Mafunzo haya yanalenga kukuza na kuimarisha uwezo na umahiri wa Wataalamu wa Ufuatiliaji na Tathmini. Ushiriki wenye mafanikio katika mafunzo haya yatamwezesha mshiriki kuendeleza, kuimarisha, na kudumisha ujuzi na umahiri wake katika:

- Kusanifu mfumo madhubuti na wenye ufanisi wa ufuatiliaji utekelezaji wa mpango mkakati.
- Kuandaa na kutekeleza mpango madhubuti wa ufuatiliaji utekelezaji wa mpango mkakati.
- Kuandaa na kutekeleza bajeti za ufuatiliaji utekelezaji wa mpango mkakati.
- Kuandaa nyenzo/zana za kukusanya data za ufuatiliaji wa mpango mkakati kwa kutumia mbinu mseto
- Kukusanya, kuchakata na kuchanganua data za ufuatiliaji utekelezaji wa mpango mkakati.
- Kuandaa taarifa za ufuatiliaji utekelezaji wa mpango mkakati za kiwango cha juu
- Kusambaza taarifa za ufuatiliaji utekelezaji wa mpango mkakati.

## WALENGWA WA MAFUNZO

Walengwa wakuu wa mafunzo haya ni pamoja na:

- Wakurugenzi, Mameneja na Maafisa Ufuatiliaji na Tathmini
- Wakurugenzi, Mameneja na Maafisa Mipango
- Wakurugenzi, Mameneja na Maafisa Miradi
- Wataalamu wa Ufuatiliaji na Tathmini
- Wadau wengine wa Ufuatiliaji na Tathmnini

## MADA KUU

Mada kuu za mafunzo haya ni pamoja na:

- **Mada 1**: Misingi mikuu na umuhimu wa ufuatiliaji utekelezaji wa mpango mkakati
- **Mada 2**: Jinsi ya kuandaa mpango na bajeti ya ufuatiliaji wa mpango mkakati
- **Mada 3:** Jinsi ya kuandaa nyenzo za ufuatiliaji utekelezaji wa mpango mkakati
- **Mada 4:** Jinsi ya kukusanya data za ufuatiliaji wa mpango mkakati
- **Mada 5:** Jinsi ya kuchakata na kuchanganua data za ufuatiliaji wa mpango mkakati
- **Mada 6:** Jinsi ya kuandaa taarifa za ufuatiliaji utekelezaji wa mpango mkakati
- **Mada 7:** Jinsi ya kuwasilisha na kusambaza taarifa za ufuatiliaji wa mpango mkakati

## MAUDHUI YA MADA KUU

- **Mada 1: Misingi mikuu na umuhimu wa ufuatiliaji utekelezaji wa mpango mkakati**
    - Utangulizi
    - Maana na umuhimu wa ufuatiliaji
    - Tofauti ya ufuatiliaji na tathmini
    - Nafasi ya ufuatiliaji katika hatua/mzunguko wa mpango mkakati
    - Majukumu makuu kwenye ufuatiliaji utekelezaji wa mpango mkakati
    - Hatua kuu kwenye ufuatiliaji utekelezaji wa mpango mkakati
    - Jinsi ya kutumia TEHAMA kwenye ufuatiliaji utekelezaji wa mpango mkakati
- **Mada 2: Jinsi ya kuandaa mfumo, mpango na bajeti ya ufuatiliaji utekelezaji wa mpango mkakati**
    - Utangulizi
    - Umuhimu wa mfumo na mpango wa ufuatiliaji utelezaji wa mpango mkakati
    - Maswali makuu ya kujiuliza wakati wa kuandaa mfumo na mpango wa ufuatiliaji utekelezaji wa mpango mkakati
    - Hatua kuu za kuandaa mfumo na mpango wa ufuatiliaji utekelezaji wa mpango mkakati
    - Jinsi ya kuandaa bajeti ya kufuatilia utekelezaji wa mpango mkakati
    - Jinsi ya kutumia TEHAMA kwenye kuandaa mfumo na mpango wa ufuatiliaji wa mpango mkakati
- **Mada 3: Jinsi ya kuandaa nyenzo za ufuatiliaji utekelezaji wa mpango mkakati na miradi**
    - Utangulizi
    - Njia na nyenzo za ufuatiliaji utekelezaji wa mpango mkakati
    - Sifa kuu za nyenzo bora za ufuatiliaji utekelezaji wa mpango mkakati
    - Jinsi ya kuandaa nyenzo za ufuatiliaji utekelezaji wa mpango mkakati
    - Jinsi ya kujaribu nyenzo za ufuatiliaji utekelezaji wa mpango mkakati
    - Jinsi ya kuboresha nyenzo za ufuatiliaji utekelezaji wa mpango mkakati baada ya majaribio
    - Jinsi ya kutumia TEHEMA kwenye kuandaa zana za ufuatiliaji utekelezaji wa mpango mkakati
- **Mada 4: Jinsi ya kukusanya data za ufuatiliaji utekelezaji wa mpango mkakati**
    - Utangulizi
    - Jinsi ya kuandaa mpango wa kukusanya data za ufuatiliaji utekelezaji wa mpango mkakati
    - Jinsi ya kukusanya data za ufuatiliaji utekelezaji wa mpango mkakati
    - Jinsi ya kutumia TEHAMA kwenye kukusanya data za ufuatiliaji utekelezaji wa mpango mkakati
- **Mada 5: Jinsi ya kuchakata na kuchanganua data za ufuatiliaji utekelezaji wa mpango mkakati**
    - Utangulizi
    - Jinsi ya kuchakata data za ufuatiliaji utekelezaji wa mpango mkakati na miradi
    - Jinsi ya kuchanganua data za ufuatiliaji utekelezaji wa mpango mkakati na miradi
    - Jinsi ya kutumia TEHAMA kuchakata na kuchanganua data za ufuatiliaji wa mpango mkakati
- **Mada 6: Jinsi ya kuandaa taarifa za ufuatiliaji utekelezaji wa mpango mkakati**
    - Utangulizi
    - Umuhimu wa taarifa za ufuatiliaji utekelezaji wa mpango mkakati
    - Aina za taarifa za ufuatiliaji utekelezaji wa mpango mkakati
    - Matumizi ya taarifa za ufuatiliaji utekelezaji wa mpango mkakati
    - Sehemu kuu za taarifa za ufuatiliaji utekelezaji wa mpango mkakati
    - Jinsi ya kundaa taarifa za ufuatiliaji utekelezaji wa mpango mkakati
    - Jinsi ya kutumia TEHAMA kwenye kundaa taarifa za ufuatiliaji utekelezaji wa mpango mkakati
- **Mada 7: Jinsi ya kuwasilisha na kusambaza taarifa za ufuatiliaji utekelezaji wa mpango mkakati**
    - Utangulizi
    - Jinsi ya kutambua walengwa wa taarifa na kukidhi matarajio yao
    - Jinsi ya kuandaa mada ya uwasilishaji wa taarifa za ufuatiliaji utekelezaji wa mpango mkakati
    - Jinsi ya kuwasilisha taarifa za ufuatiliaji utekelezaji wa mpango mkakati
    - Jinsi ya kusambaza taarifa za ufuatiliaji utekelezaji wa mpango mkakati
    - Jinsi ya kutumia taarifa za ufuatiliaji utekelezaji wa mpango mkakati
    - Jinsi ya kutumia TEHAMA kusambaza taarifa za ufuatiliaji utekelezaji wa mpango mkakati

## NJIA YA MAFUNZO

Mbinu shirikishi na ya kivitendo inayojumuisha wiki moja ya mafunzo ya ana kwa ana na ikifuatiwa na uelekezi na ushauri kwa njia ya barua pepe, WhatsApp, na simu itatumiwa katika mafunzo haya ili kuendeleza, kuimarisha, na kudumisha ujuzi na umahiri husika katika nyanja zote kuu za ufuatiliaji wa mpango mkakati. Aidha, mafunzo haya yatatumia mfumo wa TSSL wa Kujifunza, Kujaribu na Kutenda (K3).

## TAREHE ZA MAFUNZO

**Septemba – Disemba 2026**

- **Kundi A:** Septemba 14 – 18, 2026
- **Kundi B:** Oktoba 19 – 23, 2026
- **Kundi C:** Novemba 16 – 20, 2026
- **Kundi D:** Disemba 14 – 18, 2026

**Januari – Juni 2027**

- **Kundi E:** Januari 18 – 22, 2027
- **Kundi F:** Februari 15 – 19, 2027
- **Kundi G:** Machi 15 – 19, 2027
- **Kundi H:** Aprili 12 – 16, 2027
- **Kundi I:** Mei 10 – 14, 2027
- **Kundi J:** Juni 14 – 18, 2027

## SEHEMU YA MAFUNZO

Hoteli ya Morogoro iliyopo katika Manispaa ya Morogoro ndipo yatakapofanyika mafunzo haya. Ukumbi huo unatoa mazingira wezeshi kwa ajili ya matukio ya kujenga uwezo. Aidha ukumbi huo upo karibu na vivutio vya asili kwa ajili ya utalii, mapumziko, na matukio ya kujiburudisha. Baadhi ya vivutio hivi vitatembelewa na washiriki wakati wa mafunzo.

## ADA YA USHIRIKI

Ada ya usajili kwa kila mshiriki ni TZS 950,000. Ada hii **INAJUMUISHA** gharama za vitini, chai (asubuhi na jioni), chakula (mchana) wakati wa mafunzo lakini, **HAIHUSISHI** gharama za usafiri na kujikimu za mshiriki. Mwisho wa usajili ni siku 7 kabla ya kuanza kwa mafunzo.

## KUHUSU WAANDAAJI

Kampuni ya TWV Strategic Solutions Limited (TSSL) ndiyo wabunifu na waandaaji wa mafunzo haya. TSSL ni taasisi binafsi yenye makazi yake jijini Dar es Salaam na inamilikiwa na Watanzania. Washiriki wa mafunzo haya watanufaika na uzoefu mkubwa wa TSSL, wawezeshaji wake wakuu, pamoja na mtandao mpana wa ushirikiano katika utoaji wa huduma za kujenga uwezo na ufumbuzi wa kitaalamu kwa taasisi za serikali, mashirika ya umma, binafsi, na mashirika yasiyo ya kiserikali. Kwa habari zaidi kuhusu TSSL, tafadhali tembelea tovuti yetu ya www.tssl.co.tz.

## JINSI YA KUJISAJILI

- Chagua kundi la kushiriki
- Pakua fomu ya usajili kutoka kwenye tovuti yetu www.tssl.co.tz
- Jaza fomu
- Omba ankara ya malipo
- Fanya malipo ya ada kupitia tsslevents@gmail.com au WhatsApp 0754 300143
- Wasilisha fomu iliyojazwa na uthibitisho wa malipo ya ada kupitia barua pepe tsslevents@gmail.com au WhatsApp **0754 300143**